Nambari ya mtahiniwa ______________________

**S.M.Z**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**127 DINI YA KIISLAMU**

**MUDA: SAA 2:00 IJUMAA 29 /11/2019 MCHANA**

---

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. **Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, B na C. Na chagua maswali MATATU (3) kutoka sehemu D, swali la SABA (7) ni lazima. Pia chagua swali MOJA (1) kutoka sehemu E.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Andika majibu ya mtihani katika kila nafasi zilizowekwa.**

**KWA MATUMIZI YA USAHIHISHAJI TU**

| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| 12 | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 13 zenye maandishi

Nambari ya mtahiniwa ______________________

## SEHEMU A: QUR-ANI NA TAFSIRI (Alama: 20)

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Chagua jibu sahihi na andika herufi yake katika sanduku liliopo chini.

i) Aya za mwanzo kuteremshiwa Mtume Muhammad (S.A.W) ni aya:

A) Tatu (3) za Surat-Nasr. B) Mbili (2) za Suratul-Bayyinah.

C) Tano (5) za Suratul-Alaq. D) Nne (4) za Suratul-Qariyah.

ii) Mtume (S.A.W) amesema: " Mwenye kuisoma Qur-ani tukufu kwa kila herufi atapata thawabu":

A) 10 B) 20 C) 15 D) 25

iii) Neno "Id-gham" kilugha lina maana ya:

A) Kugeuza kitu kutoka hali yake kwenda hali nyengine.

B) Kuingiza kitu ndani ya kitu.

C) Kutoa kitu ndani ya kitu. D) Kuipa kila herufi haki yake.

iv) "Ole wao wale wenye kusali". Tafsiri hii ina maana ya kila:

A) Mwenye kusali nyumbani. B) Asiyesali kabisa.

C) Mwenye kusali jamaa. D) Anaesali nje ya wakati (Anaechelewesha sala).

v) Sababu ya kuteremshwa Suratul-Lahab ni kwamba Abulahab

A) Alimwambia Mtume: "Umeanngamia wewe Muhammad".

B) Alimpiga Mtume (S.A.W).

C) Alimwagia mchanga Mtume (S.A.W).

D) Alimtemea mate Mtume (S.A.W).

vi) Aya ya nne (4) ya Suratul-Lahab imeeleza kuwa mke wa Abulahab ni mchukuzi wa kuni. Aina ya kuni hizo ni kuni za:

A) Muembe. B) Mtende. C) Mninga. D) Fitina.

vii) Mke wa Abulahab alijulikana kwa jina la Ummu:

A) Salama. B) Jamil. C) Kulthum. D) Saadiya.

viii) Aya ya tano (5) ya Suratul-Falaq Allah (S.W) ametutaka tujikinge na shari za hasidi. Hasidi huyo ni yule anaetamani:

A) Neema imuondokee mwenzake. B) Azidishiwe neema mwenzake.

C) Yeye apate neema nyingi. D) Kufa kwa mwenzake.

ix) Suratul-Falaq na Suratun-Naas zinajulikana kwa jina moja liitwalo:

A) Muawidhaani. B) Muawidhuna. C) Muawidhatain. D) Muawidhina.

x) Allah (S.W) amesema katika Suratul-Lumazah " Ole wao kila mwenye kuramba kisogo". Tafsiri hii ina maana ya kila:

A) Msengenyaji. B) Mfitinishaji. C) Mpatanishaji. D) Msema uongo.

JIBU:

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. a) Panga tafsiri ya aya zifuatazo kwa usahihi wake kisha andika nambari tu.

i) Hasha bila shaka utavurumishwa katika moto wa hutwama.

ii) Anadhani kuwa mali yake itambakisha milele.

iii) Na ni jambo gani litakalokujuilisha ni nini hutwama.

iv) Ambae amekusanya mali na kuzihesabu.

v) Adhabu kali itamthibitikia kila mwenye kuramba kichogo (msengenyaji).

_______________________________________________________

b) Lete mafunzo mawili (2) yanayopatikana katika Suratul-Qariah.

_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________
_______________________________________________________

Nambari ya mtahiniwa ______________________

**SEHEMU B: TAWHIDI (Alama: 20)**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

3. Chagua jawabu kutoka orodha 'A' kwa kulinganisha kifungu cha maneno kutoka orodha 'B' na weka herufi yake kwenye sanduku liliopo chini yake.

| ORODHA "A" | ORODHA "B" |
|---|---|
| i) Kudhihirisha Uislamu na kuficha ukafiri. | a) Malaika. |
| ii) Wajumbe wa Allah (S.W). | b) Al-Muqsitu. |
| iii) Kuamini kudra ya Allah (S.W) | c) Unafiki. |
| iv) Kuchinja kwa ajili ya shetani. | d) Mitume. |
| v) Inaikomboa nafsi kutokana na shirki. | e) Imani. |
| vi) Munkar na Nakir (A.S). | f) Shirki. |
| vii) Kutoa shahada mbili. | g) Al-Badiu. |
| viii) Daud (A.S). | h) Kuandika mema na mabaya. |
| ix) Mwenye uwezo wa kuasisi. | i) Ikh-lasi. |
| x) Anaekamilisha usawa kwa viumbe. | J) Uislamu. |
| | k) Kuuliza maswali kaburini. |
| | l) Zabur. |

JIBU:

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | Viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

4. Andika herufi **"K"** kwaibara iliyokuwa sahihi na herufi **"S"**kwaibara isiyokuwa sahihi. Kisha andika herufi husika katika sanduku liliopo chini.

i) Allah (S.W) ana majina tisini na tisa (99), mwenye kuyahifadhi ataingia peponi.

ii) Kwenda kuomba katika kaburi la mtu mtukufu au walii wa Allah (S.W) sio shirki.

iii) Ria au kufanya ibada kwa kujionesha ni shirki ndogo.

iv) Mwenye imani hunyanyuliwa daraja mbele ya Allah (S.W).

v) Miongoni mwa hasara za unafiki ni kusababisha uongo katika jamii.

vi) Unafiki mdogo ni ule unaoambatana na amali za mja na kupelekea kuchafua amali zake.

vii) Kuona haya ni miongoni mwa matawi ya imani.

viii) Kutokupendana kwa ajili ya Allah (S.W) ni dalili ya mtu kukosa imani.

ix) Kuamini Nabii Issa (A.S) amesulubiwa inampelekea mja kutoka katika Uislamu.

x) Kuamini malaika wa Allah (S.W) hawali wala hawanywi ni dalili ya mtu kuwa na imani sahihi.

JIBU:

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

## SEHEMU C: HADITHI (Alama: 20)

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii**

5. Jaza nafasi zilizoachwawazi kwa kuweka maneno yaliokosekana.

i) Hadithi kilugha ni ____________________ , na kisheria ni kauli au maneno pamoja na ____________________ ambavyo Mtume (S.A.W) amevitenda.

ii) Ziko aina kuu mbili za hadithi, nazo ni hadithi __________________ na hadithi __________________.

Nambari ya mtahiniwa ____________________

iii) Hadithi ya uzuri wa imani imetoka kwa ____________________ bin ____________________ na imepokelewa na ________________.

iv) Neno سواهما lina maana ya ____________________ cha ______________________ na linapatikana katika hadithi ya ________________________________.

6. Lete tafsiri ya hadithi ifuatayo:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ، أَنَّ رَسُوْلَ اللهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ: "مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلْيَقُلْ خَيْرًا أَوْ لِيَصْمُتْ، وَمَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلْيُكْرِمْ ضَيْفَهُ، وَمَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلْيُكْرِمْ جَارَهُ" رَوَاهُ الْبُخَارِيْ.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Nambari ya mtahiniwa ______________________

**SEHEMU D:FIQHI NA MAADILI (Alama: 30)**

**Jibu maswali MATATU (3) katika sehemu hii likiwemo suala la SABA(7).**

7. Jaza mapengo yafuatayo kwa kuweka maneno yaliokosekana:

i) Udongo unaofaa kwa kutayammamu ni ule usio na ________________ wala harufu na rangi na uwe ________________________ usio changanyika na aina yeyote ya uchafu.

ii) Miongoni mwa funga za faradhi ni _________________na ___________.

iii) Zakka inayotolewa baada ya kumalizika funga ya mwezi mtukufu wa Ramadhani huitwa ____________________________________.

iv) Hadathi zimegawika sehemu kuu mbili nazo ni_________________ na _____________________.

v) Hadathi inayomsababishia mtu kukoga huitwa hadathi ___________.

vi) Nguzo za Hijja ni _____________________________ miongoni mwa hizo ni ________________________.

8. Jaza kwa usahihi nafasi zilizoachwa wazi.

a) Muislamu anatakiwa kuishi na ______________________ vizuri.

b) Ni sunna kwa Muislamu kuingia ndani ya nyumba kwa kutanguliza mguu wa _______________ hali ya _______________________ dua.

c) Miongoni mwa mambo ambayo Muislamu anatakiwa kumfanyia jirani yake ni kuishi nae kwa __________________, ___________________ na ______________________________.

d) Uasharati ni tabia ya kufanya ___________________ la ___________ kinyume na sheria za ________________________.

e) Muislamu anatakiwa _______________________ Allah (S.W) baada ya kumaliza kula.

9. Elezea tofauti iliopo kati ya sala za faradhi Aini na sala za faradhi Kifaya pamoja na kutoa mifano ya sala hizo.

10. Bainisha namna utakavyokitoharisha chombo kilichorambwa na mbwa.

**SEHEMU E : TAREKHE (Alama:10)**

**Jibu suali MOJA(1) tu katika sehemu hii:**

11. Mtume (S.A.W) alipokuwa katika jabali Hira kabla ya kupewa Utume alimshukia malaika Jibril (A.S). Fafanua namna alivyomjia Mtume (S.A.W) Malaika huyo.

12. Elezea namna Mtume (S.A.W) alivyopokelewa Madina.